


# Msaada wa Mazishi wa Coronavirus (COVID-19)

Janga la COVID-19 limesababisha huzuni kubwa kwa familia nyingi. Lengo la FEMA ni kusaidia watu kabla, wakati na baada ya misiba. Tumejitolea kusaidia kupunguza changamoto za kifedha na gharama zinazosababishwa na virusi.

**FEMA inatoa msaada wa kifedha kwa gharama za mazishi zinazohusiana na COVID-19 zilizoibuka baada ya Januari 20 2020.**



## Ili kustahiki kupokea msaada wa mazishi, ni sharti utimize masharti haya:

- Sharti kifo kiwe kimetokea Marekani.
- Anayetuma ombi sharti awe raia wa Marekani, mzaliwa au mkazi anayestahiki ambaye aligharamia mazishi baada ya tarehe 20 Januari 2020.
- Si lazima aliyeaga awe alikuwa raia wa Marekani, mzaliwa au mkazi aliyestahiki.
- Ni sharti cheti cha aliyefariki kibainishe kuwa aliaga kuhusiana na au kutokana na COVID-19. Ikiwa kifo kilitokea kati ya tarehe 20 Januari na 16 Mei, 2020 na cheti cha kifo hakihusishi kifo hicho na COVID-19, jumlisha taarifa iliyotiwa saina kutoka kwa afisa anayethibitisha cheti cha kifo, mchunguzi wa mitaa au mchunguzi wa matibabu inayohusisha kifo kutokana na COVID-19.

## Ni gharama zipi zitastahiki kufidiwa?

Mifano ya gharama zinazostahiki zinaweza kuwa pamoja na lakini sio tu:

- Usafiri ili kutambua mwili wa aliyefariki
- Kusafirisha mwili wa aliyefariki
- Sehemu ya mazishi au kuteketeza mwili
- Ishara au jiwe la kaburi
- Huduma za makasisi au waratibu
- Utumiaji wa wafanyakazi au vifaa vya makafani
- Gharama za kuteketeza au kuzika mwili

## Ninapswa kuipa FEMA taarifa zipi?

Tafadhali hakikisha kuwa una taarifa zifuatazo kabla uwasiliane na FEMA ili utume ombi:

- Jina, nambari ya ustawi wa jamii, tarehe ya kuzaliwa, anwani ya barua na nambari ya wawasiliani.
- Jina, nambari ya ustawi wa jamii, tarehe ya kuzaliwa ya kila aliyefariki.
- Eneo au mahali ambapo alipoaga.
- Hati na stakabadhi ya msaada wowote ambao tayari umepokea kutoka kwa vyanzo vingine, ikiwa ni pamoja na mazishi au bima ya mazishi, michango, mashirika ya kujitolea, mipango mingine ya serikali au mashirika yasiyo ya serikali.
- Jina na taarifa za mtuma (watuma) ombi wenza ikiwa kuna watu wengine waliogharamia mazishi ya mtu (watu) aliyefariki.

## NINAWEZAJE KUTUMA OMBI LA KUPATA MSAADA HUU?

**Piga Simu kwa Nambari ya Usaidizi wa COVID-19 wa FEMA** kwa

1-844-684-6333

(TTY: 800-462-7585)

kuanzia 9 asubuhi hadi saa 9 usiku ET, Jumatatu hadi Ijumaa na uanze mchakato wa kutuma ombi.

**Ili upokee huduma kwa haraka zaidi baada ya kutuma ombi, unaweza kuanza kutuma ombi mtandaoni kupitia**

**[Disasterassistance.gov](https://www.disasterassistance.gov), kwa njia ya faksi 855-261-3452.**

Unaweza pia kutuma barua kwa:  
Msaada wa Mazishi wa COVID-19  
S.L.P 10001  
Hyattsville, MD 20782

**Unaweza pia kututembelea mtandaoni kupitia**

**[FEMA.gov/funeral-assistance/faq](https://www.fema.gov/funeral-assistance/faq).**

Maelezo yanatolewa katika lugha mbalimbali kupitia simu na tovuti.



**FEMA**